# NATnets news

Toleo Na. 6 Machi-April 2008


## Hati Punguzo yaWatoto yafika Nchi Nzima

Utekelezaji wa mpango wa Hati Punguzo ya Watoto ulioanza mwaka 2006 katika mikoa 15 ya awali sasa umefikia katika mikoa yote 21 ya Tanzania. Mpango huu unatekelezwa kwa pamoja na mpango wa Hati Punguzo ya wajawazito ambao hauwalengi watoto moja kwa moja.

Lengo kuu la mpango wa Hati Punguzo ya Watoto ni kuwalinda watoto dhidi ya malaria kwa kuongeza upatikanaji wa vyandarua vyenye dawa kwa bei nafuu. Kila mtoto mwenye umri wa miezi 9 ana haki ya kupata hati punguzo hiyo yenye thamani ya shilingi 3,250 ambayo hutolewa kwa mtoto anapopelekwa kupata chanjo ya surua ya miezi tisa.

Hati punguzo hiyo ilianzishwa kufuatia mzigo mkubwa wa ugonjwa wa malaria kwa kundi hili lililo hatarini. Nchini Tanzania, malaria inachangia 43% ya watoto chini ya umri ya miaka 5 wanaotibiwa bila kulazwa, 35% ya watoto wanaolazwa hospitalini na 37% ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka 5. Malaria pia ni chanzo kikubwa cha upungufu wa damu kwa watoto wadogo.

Hivyo, upanuzi wa mpango huu kafikia mikoa yote nchini ni hatua kubwa katika

*(Inaendelea Uk. 4)*

## Ndani ya toleo hili:


**Ukurasa 2**
- COMMIT kuanza utekelezaji
- Tahariri

**Ukurasa 3**
- Usawa katikati upatikanaji wa vyandarua vyenye dawa

**Ukurasa 4**
- A-Z yaongeza uzalishaji Buguruni yatoa siri ya mafanikio
- Buguruni yatoa siri ya mafanikio


## Matumizi ya HP yafikia Milioni 3



Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo umepiga hatua kubwa mwezi Januari 2008 ambapo kiasi cha Hati Punguzo zinazotolewa na Mpango huo kimefikia milioni 3. Hii inamaanisha kuwa wajawazito na wakinamama wenye watoto wadogo milioni 3 wameweza kununua vyandarua vyenye dawa kupitia mpango wa Hati Punguzo.

Kwa jumla ya vyandarua milioni 6 vilivyokwishatolewa katika miaka mitatu iliyopita, mpango unahakikisha kuwa kila mjamzito na mtoto mdogo anayehudhuria kliniki atapatiwa Hati Punguzo na kujipatia chandarua chenye dawa ili kujilinda dhidi ya malaria.

Utekelezaji wa mpango huu ulianza rasmi mwezi Octoba 2004, lengo kuu likiwa kuwawezesha wajawazito na watoto kupata chandarua chenye dawa kwa bei nafuu. Kupitia mpango huu, kila mjamzito anayehudhuria kliniki ya uzazi na kila mtoto mwenye umri wa miezi 9 anapata Hati Punguzo yenye thamani ya 3,250/- sawa na theluthi mbili ya thamani halisi ya chandarua kilichofungwa na kiuatilifu. Mpango wa Hati Punguzo ni ushirikiano wa sekta binafsi na serikali, unafadhiliwa Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani.

## Rais Bush Apongeza Juhudi za Kupambana Na Malaria Tanzania

Rais wa Marekani, George W. Bush katika ziara yake ya hivi karibuni nchini Tanzania, alisifu juhudi mbalimbali za kupambana na malaria nchini. Ziara hiyo ilimpatia Rais Bush nafasi ya kujionea shughuli mbalimbali zinazofadhiliwa na Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani (PMI) na PEPFAR

Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani umekwishatoa kiasi cha dola za marekani 76.5 milioni (kwa Tanzania bara na Zanzibar) katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita ili kusaidia shughuli za kupambana na malaria.

*(Inaendelea Uk. 2)*



*Rais George W.Bush akiongea na wajawazito waliohudhuria kliniki ya uzazi katika Hospitali ya Mount Meru Arusha. Wanaotizama mbele ni Laura Bush na wahudumu wa Afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali hiyo*

# Tahariri

Tunawashukuru wasomaji wote wa jarida la Natnets kwa kulipa kimbaumbele jarida hili. Tunaendelea kupokea maoni yanayotia moyo juu ya jarida hili kutoka kwa wasomaji wetu mbalimbali.

Katika toleo hili, tunayo furaha kuwashirikisha maendeleo mapya katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo, ambao mwezi Januari 2008 ulipiga hatua kubwa pale utoaji wa hati punguzo ulipofikia kiasi cha hati milioni 3. Mafanikio haya yamewezeshwa kwa kiasi kikubwa na michango na nia ya wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na timu za vituo vya afya kama ilivyoonyeshwa katika kituo cha afya cha Buguruni.

Pia tunapenda kuchukua nafasi hii kuzungumzia ziara ya Rais George W. Bush nchini Tanzania, ziara ambayo ilituachia ujumbe mzito wa hitaji la kuwa mikakati ya kupambana na malaria inayohusisha mbinu mbalimbali kama vile matumizi ya vyandarua vyenye dawa, dawa mseto za malaria na upuliziaji wa dawa majumbani pamoja na mikakati mingine.

Nia ya serikali na wadau katika kuhakikisha upatikanaji wa vyandarua vyenye dawa kwa kuzingatia usawa hasa kwa makundi yaliyo katika hatari kubwa ya malaria ni ya muhimu pia. Mbinu hii mpya inayosaidiana na mpango wa Hati Punguzo, inayolenga kuwafikia watoto wenye umri chini ya miaka 5 kupitia kampeni maalum, itahakikisha kuwa watoto ambao hawajafikiwa na mpango wa Hati Punguzo wanalindwa kwa chandarua chenye dawa ya kudumu. Hatua ya kiwanda cha A-Z kuongeza uzalishaji wa vyandarua vyenye dawa ya kudumu ni kielelezo kuwa hata sekta binafsi haijaachwa nyuma katika vita dhidi ya malaria.

Tunawashukuru MEDA kwa kufadhili toleo hili la jarida la Natnets

**NATnets News imetolewa na**
ITN Cell
Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria
S. L. P. 3430
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2124 977
Nukushi: +255 22 2124 976
Barua-pepe: info@natnets.org

**Imeandaliwa na**
MediaNet Limited
S. L. P. 8608
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2760 288
Barua-pepe: info@medianettz.com

# Rais Bush Apongeza Juhudi za Kupambana Na Malaria Tanzania

*(Inatoka Uk. 1)*

Msaada huo umekuwa ukiongezeka kila mwaka ambapo kiasi cha juu kilichowahi kutolewa ni dola za marekani 34 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kupambana na malaria Tanzania bara na Zanzibar kuanzia mwezi Octoba 2007 hadi Septemba 2008.



*Rais George Bush akitoa chandarua chenye dawa kwa mama mjamzito katika Hospitali ya Mount Meru*

Wakati wa ziara hiyo, Rais Bush alitangaza kuwa mwaka huu PMI itajiunga na Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Benki ya Dunia katika kusambaza vyandarua vyenye dawa ya kudumu milioni 5.2 kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka 5 Tanzania Bara. Rais alipata nafasi ya kutembelea vituo mbalimbali mkoani Dar es Salaam na Arusha.

Akiwa mkoani Arusha, alishuhudia uzalishaji wa vyandarua vyenye dawa ya kudumu katika kiwanda kilichoanzishwa kwa ubia baina ya kiwanda cha nguo cha A-Z na kampuni ya kimataifa ya Sumitomo Chemicals kutoka Japan.

Pia alitembelea kliniki ya uzazi na wodi ya watoto katika hospitali ya Mount Meru ambapo watoto wenye malaria hupatiwa huduma. Akiwa katika hospitali hiyo, Rais Bush alipata nafasi ya kuzungumza na wajawazito waliokuwa wakisubiri huduma ya kliniki ya uzazi na kujionea namna Hati Punguzo zinavyotolewa kwa wajawazito hao. Pia alitoa vyandarua vyenye dawa kwa baadhi ya wajawazito katika hospitali hiyo.

Katika risala yake hospitalini hapo, Rais Bush alieleza haja ya kuwa mbinu za ushirikiano katika kupambana na malaria, akatoa mfano wa Zanzibar na wilaya ya Muleba, ambapo mafanikio makubwa yamepatikana katika kupunguza mzigo wa malaria kwa makundi yaliyo hatarini kufuatia uanzishwaji wa upuliziaji wa dawa majumbani pamoja na matumizi ya vyandarua vyenye dawa na dawa mseto za malaria.

# COMMIT kuanza Utekelezaji

Mnamo tarehe 3 Machi 2008, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP) kwa kushirikiana na wadau wengine, uliandaa mkutano wa majadiliano uliowahusisha wadau wa Mradi wa Malaria na Mawasiliano, kwa nia ya kupata mawazo kutoka kwa wadau hao ili kufikia makubaliano ya pamoja juu ya utekelezaji wa mradi. Waliohudhuria ni pamoja na maafisa kutoka Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria, Chuo cha Afya ya Kijamii cha John Hopkins Bloomberg, PSI-Tanzania, Taasisi ya Utafiti ya RTI, Shirika la Misaada la Marekani (USAID)/ Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani (PMI), JHPIEGO, wawakilishi kutoka viwanda vinavyotengeneza vyandarua na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mkutano huo ulilenga kuchambua tabia zinazotakiwa kuhamasishwa pamoja na ujumbe mahususi utakaofikishwa katika jamii kwa nia ya kuhamasisha matumizi ya vyandarua vyenye dawa, utafutaji wa huduma za afya kwa wakati unaofaa pamoja na matibabu sahihi ya malaria kwa kutumia dawa mseto za malaria, kinga ya malaria wakati wa ujauzito, upuliziaji wa dawa za mbu majumbani pamoja na mbinu zingine za kujikinga na malaria zinazotumika nchini.

Lengo kuu la mradi wa COMMIT ni kuongeza nguvu katika mikakati ya kupambana na malaria inayoendelea kwa kuhakikisha kuwa jamii za Tanzania, kaya zake na watu binafsi wanapatiwa elimu pamoja na ujuzi muafaka juu ya ugonjwa wa malaria ili waweze kutumia njia zilizopo za kuokoa maisha yao. Mkazo mkubwa utawekwa katika kuyafikia makundi yaliyosahaulika katika upatiwaji wa taarifa muhimu hasa wale waishio vijijini.

Mradi huu utatekelezwa kwa njia ya ushirikiano baina ya Chuo cha Afya ya Kijamii cha John Hopkins Bloomberg, PSI- Tanzania na Taasisi ya Utafiti ya RTI. Unafadhiliwa na PMI.

# Usawa katika upatikanaji wa Vyandarua vyenye Dawa…..

## Watoto chini ya miaka 5 kupata vyandarua bila malipo

Kwa miaka mingi, mtazamo wa serikali na wadau wa maendeleo umekuwa katika kutafuta njia bora ya kupunguza mzigo wa malaria baina ya makundi yaliyo hatarini hasa wajawazito na watoto chini ya miaka 5. Uanzishwaji wa Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo ulikuwa ni hatua kubwa katika kuwaongezea wajawazito na watoto wao upatikanaji wa vyandarua vyenye dawa kwa bei nafuu.

Kupitia mpango huo, kila mjamzito anayehudhuria kliniki ya uzazi pamoja na mtoto mwenye umri wa miezi tisa wanapatiwa Hati Punguzo yenye thamani ya shilingi 3,250 ambayo ni theluthi mbili ya bei halisi ya chandarua kilichofungwa na viuatilifu. Mtoto anapotimiza umri wa miezi tisa hupatiwa Hati Punguzo anapokwenda kliniki kwa ajili ya chanjo ya surua.



Picha na M. Hallahan

Pamoja na juhudi hizi, bado kuna changamoto zinazotakiwa kufanyiwa kazi ili kuongeza upatikanaji wa vyandarua vyenye dawa pamoja na kuhakikisha kuwa kuna usawa katika kuyalinda makundi haya yaliyo katika hatari ya malaria.

Matokeo ya awali yaliyotokana na tathmini ya Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo yanaonyesha kuwa pamoja na kuwepo kwa ongezeko la umilikaji wa vyandarua vyenye dawa katika makundi yote, tofauti ya ufikiwaji baina ya matabaka ya kiuchumi na kijamii bado inaonekana. Wanawake na watoto walio maskini zaidi bado wana nafasi ndogo ya kutumia chandarua chenye dawa na ufikiwaji bado ni mdogo maeneo ya vijijini.

Wakati Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo unasisitiza kuwa chandarua chenye dawa kitakachopatikana kupitia Hati Punguzo ya Watoto kitadumu kwa miaka miwili, namna ya kumlinda mtoto kati ya miaka 3 na 5 bado ni swala la kuzingatia.

Kufuatia hali hiyo, serikali ya Tanzania kwa msaada wa Benki ya Dunia, Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani (PMI) na Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu inapanga kusambaza vyandarua vyenye dawa ya kudumu kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka 5 bila malipo kwa kupitia kampeni maalum. Ufikiwaji wa watoto pia unaendelea kupitia Hati Punguzo ya Watoto inayofadhiliwa na Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani (PMI). Thamani ya Hati Punguzo ya wajawazito na ya watoto chini ya miaka 5 pia itaongezwa ili kupunguza gharama za kuongezea ili kuyawezesha makundi yaliyo maskini zaidi kujinunulia chandarua chenye dawa ya kudumu.

## Tuliyojifunza kutokana na Hati Punguzo ya Usawa

Mwezi Septemba 2006, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, ilianzisha Hati Punguzo ya Usawa kama sehemu ya juhudi zinazoendelea za kuhakikisha usawa katika upatikanaji wa Vyandarua vyenye Dawa kwa makundi yaliyo katika hatari ya malaria. Uanzishwaji wa Hati Punguzo hiyo, unatokana na ripoti kutoka katika sehemu mbalimbali za nchi zinazoonyesha bado idadi kubwa ya wajawazito na watoto wao hawawezi kumudi kiasi cha bei ya kuongezea ili kupata chandarua chenye dawa pamoja na kuwa na Hati Punguzo. Wilaya sita ikiwa ni pamoja Tandahimba, Nachingwea, Bagamoyo, Magu, Dodoma vijijini na Sumbawanga vijijini, zilichaguliwa kwa ajili ya majaribio ya mpango huo kutoka na kuwa vifo vingi vya watoto wachanga na wenye umri chini ya miaka mitano pamoja na kiwango cha juu cha umaskini.

Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huo una maendeleo madogo na unakabiliwa na changamoto nyingi katika kuwafikia walengwa. Changamoto hizo ni pamoja na tafsiri sahihi ya nani ni maskini, kutokana na kubadilika kutoka eneo moja hadi lingine, ukosefu wa utaratibu wa kutegemewa wa kuwatambua walio maskini zaidi, utaratibu mbovu wa uwekaji kumbukumbu katika jamii pamoja na ugumu wa kuratibu njia za usambazaji wa Hati Punguzo.

Changamoto hizi zinatoa mwanga kwa kampeni maalum inayokuja ya kuwafikia watoto wenye umri chini ya miaka mitano itakayotekelezwa kupitia katika jamii. Watoto wanaostahili kupatiwa chandarua chenye dawa ya kudumu wataandikishwa na wafanyakazi wa serikali za mitaa katika ngazi za kata na vijiji.

## Hati Punguzo au vyandarua bila malipo

Uamuzi wa serikali wa kusambaza vyandarua vyenye dawa ya kudumu bila malipo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kupitia kampeni maalum sanjari na utekelezaji wa mpango wa Hati Punguzo ni uamuzi mkubwa. Uamuzi huu unatokana na majadiliano marefu ya miaka mingi juu ya njia bora ya kuhakikisha upatikanaji wa vyandarua vyenye dawa kwa makundi yaliyo hatarini kama njia ya kupambana na malaria.

Kwa upande mmoja wapo wanaokubaliana na usambazaji wa vyandarua bila malipo, wakionyesha umuhimu wa usawa na usambazaji mpana wa vyandarua hivyo vinavyoweza kuokoa maisha. Kwa upande mwingine ni wale wanokubaliana na mfumo wa uchangiaji wa gharama kama ilivyo Hati Punguzo na kusisitizia hitaji la kuwa na mkakati endelevu kwa kuihusisha sekta binafsi na kuhamasisha matumizi ya vyandarua vyenye dawa.

Mfumo wa uchangiaji kama ule wa Hati Punguzo unalenga kuweka utaratibu endelevu ambao unawawezesha wazalishaji kutimiza mahitaji mahitaji ya jamii. Kwa upande wa wahitaji gharama ndogo wanazochangia huwafanya kutambua umuhimu wa kinga hiyo, na hivyo uamuzi wao wa kununua vyandarua utalenga kuhakikisha kuwa wajawazito na watoto wanalala ndani ya chandarua chenye dawa wakati wote. Kwa upande wa wazalishaji, uzalishaji na usambazaji hutekelezwa kupitia sekta binafsi ambayo kwa shughuli hizi ina ufanisi zaidi ya serikali.

Mfumo wa usambazaji wa vyandarua bila malipo una maana ya kuwa serikali ndiyo yenye wajibu wa kuhakikisha kuwa kila mlengwa anapatiwa chandarua bila malipo. Pia una maana ya kuwa serikali itakuwa na uwezo endelevu wa kudhamini na kutoa msaada wa kitaalam unaohusiana na shughuli hii. Dhana hii inaiachia serikali kutoa maamuzi yote juu ya maswala ya gharama za kifedha.

Aidha, pande zote mbili zinahitaji kupongezwa kwa mawazo na misimamo yao ambayo imewezesha kutumia mfumo wa sasa ambao unatambua umuhimu wa kusisitizia mfumo uliopo wa Hati Punguzo pamoja na kampeni maalum ya mara moja inayolenga kuwafikia watoto wote ambao hawafaidiki na mpango wa Hati Punguzo.

# Hati Punguzo yaWatoto yafika Nchi Nzima

*(Inatoka Uk. 1)*

kuhakikisha kuwa kundi hili lililopo hatarini linakingwa dhidi ya malaria. Mikoa 6 itakayofikiwa ni Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Singida na Tabora. Maafisa wa mafunzo kutoka World Vision Tanzania wamekwisha wasili katika mikoa yote 6 na wanatoa mafunzo kwa wahudumu wa Afya ya Mama na Mtoto katika vituo mbalimbali. Mafunzo hayo yanakwenda sanjari na usambazaji wa Hati Punguzo za Watoto katika vituo vya afya unaofanywa na wafanyakazi waliopatiwa mafunzo kutoka MEDA.

Hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi 2008, vituo vya afya 106 kati ya vituo 705 katika mikoa hiyo sita vilikwisha fikiwa. Inategemewa kuwa vituo vilivyobaki vitakuwa vimefikiwa ifikapo mwishoni mwa Aprili. Mafunzo yanalenga angalau wahudumu 3 wa Afya ya Mama na Mtoto katika ngazi ya Zahanati, wahudumu 5 katika Kituo cha Afya na 10 katika ngazi ya hospitali.

Njia iliyotumiwa ya kuwapatia mafunzo wahudumu wakiwa katika vituo vyao vya kazi, imerahisisha kuwapatia mafunzo wahudumu wengi kwa pamoja huku wakiendelea na shughuli zao za kawaida. Pia imewezesha wakufunzi kusimamia shughuli zingine za Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo katika vituo hivyo huku wakiwapatia wahudumu wa Afya ya Mama na Mtoto maendeleo mapya mpango huo.

Mpango wa Hati Punguzo ya Watoto unafadhiliwa na Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani kupitia Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

# Kituo cha Afya cha Buguruni chatoa Siri ya Mafanikio

*Kituo cha Afya cha Buguruni ni moja ya vituo vya afya vya Dar es Salaam ambavyo vimekuwa na mafanikio katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo. Kutoka mwezi Octoba 2004 hadi sasa, kituo kimetoa Hati Punguzo kwa wajawazito zaidi ya 12,000. Katika toleo hili tunazungumza na Dkt. Mwajuma Mbaga, Mganga Mkuu wa Kituo, juu ya sababu zinazofanikisha mpango huo katika kituo chao.*

Swali na Jibu

**S: Ni sababu gani zinazopelekea wajawazito wengi kujitokeza kuchukua Hati Punguzo katika kituo chenu?**

**J:** Kujitokeza kwa wingi kwa wajawazito kuchukua Hati Punguzo katika kituo chetu, kunachangiwa na juhudi za pamoja za uongozi wa kituo, watoa huduma na wadau wengine katika kuhakikisha kuwa wajawazito wanahamasishwa kuhudhuria kliniki za uzazi na mtoto ambapo hupatiwa Hati Punguzo. Pia tumejitahidi kuboresha huduma za afya katika kituo kama vile usafi, elimu ya afya ya jamii, na utoaji wa huduma za rufaa za uhakika pale inapolazimu. Hii imesaidia kuwavutia wajawazito wengi kuja katika kituo chetu.

Kwa kuongezea, kituo kimejengwa katika eneo linalofikika kirahisi hivyo wajawazito wote kutoka Kata ya Buguruni wanaweza kufika kwa urahisi.

**S: Je, mnawafikiaje wajawazito nje ya kituo chenu?**

**J:** Tunao mpango mahususi wa kuwafikia wajawazito nje ya kituo, unaowahusisha watoaji huduma za afya katika jamii, vikundi vya vijana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi katika jamii. Wadau hawa wamekuwa chachu katika kuwaelimisha wajawazito juu ya Mpango wa Hati Punguzo na udhibiti wa malaria kwa ujumla.

**S: Ni changamoto gani zinazowakabili katika utekelezaji wa Mpango wa Hati Punguzo?**

**J:** Kiasi cha bei ya kuongezea katika Hati Punguzo bado ni changamoto kubwa. Tunafanya jitihada kubwa za kuifikia jamii, na kuwahamasisha wanaume kuwasaidia wake zao kumudu kiasi cha bei ya kuongezea kati Hati Punguzo.



*Dkt Mwajuma Mbaga*

# A-Z kuongeza Uzalishaji wa Vyandarua Vyenye Dawa ya Kudumu



*Picha na M. Hallahan*

Kiwanda kinachoongoza kwa uzalishaji wa vyandarua vyenye dawa Tanzania cha A-Z, hivi karibuni kilizundua kiwanda kipya cha kisasa cha kutengeneza vyandarua vyenye dawa ya kudumu. Kiwanda hicho ni ubia kati ya A-Z na kampuni ya kimataifa ya kemikali iitwayo Sumitomo kutoka Tokyo.

A-Z ilianza kwa kuingiza technologia kutoka nje na sasa kimekuwa kiwanda kikubwa na pekee Afrika kinachozalisha vyandarua vyenye dawa ya kudumu huku kikiwa na uwezo mkubwa wa uzalishaji. Kwa kuzindua kiwanda hicho kipya, A-Z inapanga kuzalisha angalau vyandarua milioni 10 kwa mwaka. Hadi sasa kiwanda kimetoa nafasi za ajira 3,200, zinazosaidia zaidi ya watu 20,000.

Wakati wa uzinduzi wa kiwanda hicho kipya mnamo tarehe 8 Februari 2008, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Dkt. Ali Mohamed Sheih alikisifu kiwanda cha A-Z kwa mchango wake katika kupambana na malaria na kupunguza umaskini. Pia alielezea umuhimu wa vyandarua vyenye dawa kama njia bora na isiyo na gharama kubwa ya kujikinga dhidi ya malaria.

Vyandarua vyenye dawa ya kudumu vya Olyset®, ambavyo ni bidhaa inayotengenezwa na A-Z vinasifiwa kwa uimara na kudumu kwa muda mrefu. Ndio chandarua cha kwanza chenye dawa ya kudumu kilichothibitishwa na kitengo cha kutathmini dawa za kuulia wadudu cha Shirika la Afya la Dunia (WHOPES).

Vyandarua vya Olyset® hushonwa katika namna ambayo kinaweza kupitisha hewa ya kutosha bila mbu kupita. Vyandarua hivi huwekwa dawa kiwandani na hubaki na nguvu ya kuua mbu hata baada ya kukifua mara kwa mara. Hivyo hakihitaji kuwekwa dawa tena na hudumu kwa miaka mitano.

Wadau wetu

Wahisani wetu

World Bank